

## KAZI YA LIKIZO

### KISWAHILI KIDATO CHA 5

1. Msanii hutumia mitindo mbalimbali kutia ladha na kupevusha ujumbe uliopo katika kazi zao. Kwa kutumia vitabu viwili vya riwaya jadili jinsi mitindo ilivyotumika kupevusha ujumbe. Toa hoja nne kwa kila kitabu.
2. Fasihi simulizi ili iweze kutendeka hutawaliwa na mambo makuu Matano. Kwa mifano Dhahiri fafanua mambo hayo.
3. Kwa mifano Dhahiri fafanua matokeo hasi ya kuwepo kwa hali ya mtu kugharamia kitu Fulani kisicho chake kwa kutoa msaada. Toa hoja tano kuonesha uhasi huo.
4. Utamu wa uwasilishaji wa kazi za fasihi andishi hutokana na mchango mkubwa kutoka katika fasihi simulizi. Thibitisha ukweli wa kauli hiyo ukitumia mifano mbalimbali ya kazi za fasihi andishi. (Hoja tano (5)).
5. “Lengo la hadhira katika kazi ya fasihi ni kuipa uhai kazi husika”. Fafanua dhima tatu za hadhira katika upande wa hadithi na dhima mbili za hadhira katika utanzu wa vitendawili.
6. Dhamira ya mapenzi ni moja ya dhamira inayowafikirisha waandishi. Kwa kutumia hoja nane kutoka katika riwaya ya MFADHILI thibitisha kauli hiyo.
7. Eleza maana ya ngano. Kisha fafanua faida nne (4) za maneno ya kifomula kama sifa mojawapo ya ngano.
8. Jadili dhana ya fadhila kama ilivyojitokeza katika kitabu cha MFADHILI. Tumia hoja nane kwa kila kitabu.
9. “Watetezi wa nyakati zako wanasulubiwa kabla ya kuonesha suluhisho alilokusudia mwandishi”. Fafanua hoja hiyo ukihusisha tamthiliya mbili (Hoja nne kwa kila hoja)
10. Tamthiliya ulizosoma zimepitwa sana na wakati. Jadili ukweli wa kauli hii kwa kutumia tamthiliya mbili ulizosoma (Toa hoja nne kwa kila hoja)

### KISWAHILI I

1. (a) Nini maana ya alofoni?  
(b) Jadili mazingira ya utokeaji wa alofoni
2. “Kila sentensi ni tungo lakini si kila tungo ni sentensi”. Thibitisha kauli hii kwa hoja tano.
3. Jadili hali tano za vitenzi vya Kiswahili kwa kutumia mifano.
4. Bainisha tofauti zilizopo baina ya kirai na sentensi. (Toa hoja tano).
5. Jadili mchango wa siasa katika kukua na kuenea kwa kiswahii nchini Tanzania baada ya uhuru (Toa hoja sita).
6. “Kiswahili ni Kiarabu kwa jina lakini ni Kibantu kwa dhati”. Thibitisha kauli hii kwa hoja tano za kiisimu.
7. “Ukalimani na tafsiri ni mapacha wasiofanana”. Thibitisha kauli hii kwa hoja sita.